



Tovuti: [www.nsimbodc.go.tz](http://www.nsimbodc.go.tz)

# Nsimbo Wiki hii

Tunatekeleza .....

TOLEO NA.03

FEBRUARI 16, 2019

## Mil.18 zanufaisha vikundi vya Ujasiriamali Nsimbo

- ◆ *Ni kati ya zile asilimia 10 kwa ajili ya Wanawake, Vijana na Wenye Ulemavu,*
- ◆ *Wapatiwa mafunzo namna ya kutumia fursa hiyo,*
- ◆ *Watakiwa kuzingatia muda wa marejesho*



**Na :John Mganga –NDC**

*Nsimbo -Makao Makuu*

Vikundi vya Ujasiriamali vya Vijana, wanawake na Walemavu kutoka katika kata 12 za Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo wamenufaika na Shilingi Mil 18 ikiwa ni asilimia 10 ya fedha ya makusanyo ya ndani kwa robo ya pili ya mwaka wa fedha 2018/2019.

**Zaidi endelea Uk. ...2**

*Fundi wa Vifaa vya TEHAMA kutoka Kampuni ya SATCOM Africa Bw.Ruben aki-funga V-Sat Dish mpya na ya kisasa zaidi katika eneo la Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo Februari 15,2019.Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo imekuwa ikifanya Mawasiliano na OR-TAMISEMI ili kuboreshewa Miundombinu ya TEHAMA .Picha na John.Mganga)*

## TAMISEMI yaimarisha Mtandao Nsimbo

**Na:Mwandishi wetu-NDC**

Changamoto ya kasi ndogo ya Mtandao iliyokuwa ikiathiri kwa kiasi kikubwa shughuli mbalimbali za utoaji huduma kupitia mifumo ya TEHAMA Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo imepatiwa mwarobaini, Afisa Habari na Kaimu Mkuu

wa Kitengo cha Teknolojia ya Habari, Mawasiliano na Uhusiano Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo **Bw.John Mganga** ameeleza .

Bw.Mganga ameyasema hayo Februari 11, 2019 ofisini kwake ambapo ameeleza kuwa maboresho hayo ni jitihada za Serikali kupitia Wizara ya TAMISEMI kuboresha miundombinu

ya TEHAMA ili kuharakisha utoaji huduma kwa Wananchi.

Katika maboresho hayo Nsimbo imefungiwa Mfumo wa Mawasiliano wa V-Sat Dish ulioboreshwa zaidi unaoweze-sha Mifumo ya TEHAMA kufanya kazi kwa kasi ya kuridhisha na kiwango kinachotakiwa.

**Inaendelea Uk.....3**

### YALIYOMO;

- ◆ **Mwenyekiti 3**  
*Nsimbo alani sham-bulizi Diwani Kapalala...*
- ◆ **Mwenge wa 4**  
*Uhuru kutua Nsimbo Aprili ,2019... ..*
- ◆ **Ofisi ya RAS 5**  
*Katavi yafan-ya Ukaguzi Mfumo wa Ukusanyaji*

## Mil 18 zanufaisha Vikundi ya Ujasiriamali Nsimbo.....Inatoka uk 1

Kaimu Afisa Maendeleo ya Jamii Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo **Bw.AlexW. Magesa** ameeleza kuwa fedha hizo zilizokabidhiwa kwa Vikundi vya Ujasiriamali vya Vijana, wanawake na Wenye ulemavu zimetokana na Makusanyo ya ndani pamoja na Mfuko wa Marejesho.

**Magessa** ameliambia Nsimbo Wiki hii kuwa tayari fedha hizo zimekwisha kuingizwa katika Akaunti za Vikundi hivyo kwa ajili ya kuwawezesha kufanya shughuli zao mbalimbali za Ujasiriamali.

Februari 8, 2019 Vikundi vya

Wajasiriamali Vijana, akina mama na Wenye Ulemavu kutoka katika Kata zote za Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo vilipewa mafunzo kwa ajili ya kujenga uwezo wa namna ya kutumia fedha za Mkopo kujikwamua kiuchumi.

Mafunzo hayo yalilenga pia kujenga uelewa juu ya muhimu wa Wajasiriamali hao kuzingatia marejesho pindi wachukuapo Mikopo ili kusudi mikopo hiyo iweze kuwa na tija na manufaa zaidi kwao na kwa vikundi vingine vya Ujasiriamali.

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa mafunzo hayo **Bw.Magessa** alitoa wito kwa Vikundi vya Wajasiriamali Wilayani Nsimbo, kuhakikisha kuwa wanatumia fedha wanazokopa vizuri ikiwa ni

pamoja na kuwa na mawazo sahihi ya Biashara ili mikopo wanayopata iweze kuwanufaisha na pia waweze kufanya marejesho kwa wakati.

Ameleza kuwa kutokufanya Marejesho kwa wakati kwa Baadhi ya vikundi vya Ujasiriamali Nsimbo kumekuwa sababu mojawapo inayokwamisha utoaji kwa wa Mikopo kwa wakati hali inayoathiri utekelezaji wa malengo mahsusi ya serikali ya kuwawezesha Kiuchumi wanawake, Vijana na Wenye Ulemavu.

Aidha Magesa ameeleza kuwa Utoaji wa Mikopo kwa wakati Nsimbo umekua ukiathiriwa zaidi na kushuka kwa mapato ya Halmashauri ambapo ameeleza kuwa kwa mwaka wa fedha 2018/2019 Shilingi Mil.115 za makusanyo ya ndani zilitengwa ikiwa ni Asilimia 10 kwa ajili ya kuwezesha Wanawake, Vijana na Wenye Ulemavu.

Magesa amesema kuwa kutofikiwa kwa malengo ya utoaji wa asilimia 10 kama ilivyotengwa katika Bajeti kumeathiriwa zaidi na kushuka kwa mapato ya ndani hali inayolazimu Halmashauri kutenga 10% ya kile kilichokusanywa kwa ajili ya Shughuli za Ujasiriamali kwa Vijana, wanawake na Wenye Ulemavu wakati harakati za kuboresha ukusanyaji wa mapato zikiendelea.



*Pichani: Afisa Maendeleo ya Jamii Bi. Dianarose Munuo akitoa mafunzo ya namna ya kutumia fedha za Mikopo kwa Wajasiriamali Wanawake, Vijana na Wenye Ulemavu katika ukumbi wa Mikutano wa Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo Februari 9, 2019 kabla ya kuingiziia fedha hizo. Kwenye akaunti zao (Picha na John Mganga-NDC)*

## TAMISEMI yaimarisha Mtandao Nsimbo .....Inatoka uk 1

Mganga ameeleza kuwa awali Nsimbo ilikuwa ikitumia mfumo huo huo wa Mawasiliano ya V-Sat Dish ambao ulikuwa na changamoto kadhaa hususani wakati wa kipindi cha mvua ambapo kasi ya mtandao ilikuwa ni ndogo hali iliyosababisha kupungua kwa kasi ya utiaji huduma za Kimifumo.

Kutokana na changamoto hiyo Februari 11 Ofisi ya Rasi TAMISEMI ilituma vifaa kwa ajili ya maboresho ya Mfumo huo wa Mawasiliano ambapo tayari Fundi kuoka Kampuni ya Satcom Africa amekwishafunga V Sag Dish mpya ambayo ina uwezo mkubwa tofauti na ya mwanzo ambayo ilikuwa na changamoto kadhaa.

Maboresho hayo yameongeza maradufu kasi ya mtandao ambapo mara baada ya kukamilika kwa zoezi la ufungaji wa Vi Sat Dish mpya watumiaji wa Mfumo ya Mapato wameeleza kufurahishwa kwao na kasi ya mtandao iliyopo sasa tofauti na ya awali.

## Mwenyekiti Nsimbo alaani shambulizi la Diwani Kapalala

**Na:John A.Mganga**

*Nsimbo-Kapalala*

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo **Mh.Raphael Kalinga** amelaani vikali tukio la kuvamiwa na kushambuliwa kwa mapanga kwa Diwani wa Kata ya Kapalala **Bw.Reward Sichone**.

Tukio hilo lilitokea usiku wa kuamkia Februari 12, katika Kijiji cha Mtakuja katika eneo la Bar maarufu kwa jina la Chuichui mita Chache kutoka Nyumbani kwa Diwani Sichone ambapo kwa mujibu wa maelezo yake katika Mahojiano na Nsimbo Wiki hii,Watu wenye mapanga,wanaosadikiwa kuwa ni majambazi walimvamia Diwani Sichone baa hapo wakati akienda Msalani na kuanza kumshambulia kwa mapanga.

Akizungumza na waandishi wa Habari Mwenyekiti Kalinga

amesema tukio la kuvamiwa na kushambuliwa kwa diwani sichone ni la kikatili na kwamba ni kitendo kisichokubalika katika Jamii

Amesema matukio ya kihalifu ya Uvamizi na uporaji yamekuwa yakifanywa kwa sehemu kubwa na Makundi ya kihalifu hususani Vijana ambao kutokana na kukosa shughuli za kufanya wamekuwa wakijihusisha na matukio ya wizi na uporaji wa mali za watu.

Mwenyekiti Kalinga ametoa wito kwa vijana kuachana na tabia za uporaji na badala yake kutafuta fursa mbalimbali za ajira halali zitakazowawezesha kujikwamua na umasikini badala ya kujihusisha na vitendo vya kihalifu vinavyohatarisha uhai wa maisha yao.

Ametoa wito kwa vyombo vya usalama kuhakikisha kuwa wanasaka watuhumiwa wote wanaojihusisha na vitendo vyaukatili na wizi na kuwafikisha katika vyombo

vya sheria ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa.

Kalinga ameeleza kuwa Usalama wa Raia na mali zao ni chachu ya maendeleo ya Jamii kwa kuwa palipo na amani na utulivu jamii huzingatia zaidi shughuli za uzalishaji badala ya taharuki inayowafanya kutoshiriki katika shughuli za kiuchumi za ujenzi wa Taifa

Diwani huyo wa Kata ya Kapalala anapatiwa matibabu katika Zahanati ya Nsimbo ambapo mpaka hivi sasa anaendelea vema na matibabu kutokana na wataalamu wa Zahanati hiyo ya Nsimbo kuthibitisha kuwa anaweza kuendelea na matibabu hapo hapo mpaka atakaporuhusiwa.



# Mwenge wa Uhuru kutua Nsimbo Aprili, 2019



*Pichani : Aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Katavi Meja Jenerali Mstaafu Raphael Muhuga (Kulia aliyevaa Kapelo Nyeupe) alipokabidhiwa Mwenge wa Uhuru na Mkuu wa Mkoa wa Tabora Mh. Agrey Mwanri May 2, 2018 katika Uwanja wa Ndege Mpanda. Kabla ya kukimbizwa Katika Halmashauri za Mkoa wa Katavi (Picha na Maktaba Nsimbo HQ)*

## **Na John Mganga-NDC**

*Nsimbo- Makao makuu*

Mwenge wa Uhuru wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania unatarajia kuwasili Nsimbo Aprili 13, 2019, mratibu wa Mwenge Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo Bw. Alex Wema Magessa amedokeza.

Magessa ameeleza kuwa taarifa za kuwasili kwa Mwenge wa Uhuru wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Nsimbo ni kwa mujibu wa ratiba ya Shughuli za Mwenge iliyotolewa na Ofisi ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera Bunge, Kazi Vija-na, Ajira na Wenye ulemavu.

Mratibu wa Mwenge Nsimbo ameeleza kuwa Mapokezi ya Mwenge wa Uhuru kwa mwaka huu 2019 yatakua ya aina yake kutokana na namna ambavyo Ofisi yake imelipa uzito wa kipekee suala hilo.

Amesema kuwa kwa sasa Nsimbo inaandaa miradi itakayozinduliwa na Mwenge na kwamba Ofisi yake itaendelea kuwajua Wananchi hatua mbalimbali za maandalizi ya Mapokezi ya Mwenge wa Uhuru.

Aidha ameongeza kuwa Miradi itayozinduliwa Nsimbo kwa mwaka huu ni miradi ya Kihistoria kwa kuwa inalenga kui-

marisha zaidi utoaji huduma kwa Wananchi.

Kwa mwaka 2018 mwenge wa Uhuru uliwasili Nsimbo na kupokelewa katika Kijiji cha Mtapenda Kata ya Mtapenda Aprili 4, 2018 na kuzindua miradi mbalimbali ya maendeleo ambapo ulikabidhiwa katika uwanja wa Mpira wa Kanoge kabla ya kukabidhiwa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Mpimbwe.

## Ofisi ya RAS Katavi yafanya Ukaguzi Mfumo wa Ukusanyaji Mapato Nsimbo.

**Na: John Mganga**

*Nsimbo -Makao Makuu*

Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Katavi kupitia Afisa TEHAMA wa Mkoa Februari 15, 2019 imefanya Ukaguzi wa Mfumo wa Ukusanyaji wa Mapato LGRCIS ili kubaini chanamoto mbalimbali za Mfumo huo.

Afisa TEHAMA wa Mkoa wa Katavi Bw.Curthbert Swai ameeleza kuwa Ukaguzi huo unafanyika ikiwa ni maelekezo kutoka Ofisi ya Rais TAMISEMI kufanya ukaguzi wa Mifumo ili kiubaini changamoto mbalimbali zinazotokea lengo likiwa ni kufanya maboresho ya Mfumo huo.

Ameleza kuwa Ukaguzi wa Mfumo wa Mapato una lengo la kuimarisha Ukusanyaji wa mapato pamoja na suala zima la udhibiti.

Bw.Swai ameeleza kuwa Ukaguzi wa Mifumo mbalimbali ni zoezi endelevu na kwamba linafanyika kwa lengo la kubaini mapungufu mbalimbali yanayotokea katika matumizi ya Mifumo hiyo ili kuweza kubaini na baadae kuchukua hatua madhubutii kukailiana na changamoto hizo

Akiwa Nsimbo Bw.Swai amekagua Mashine za Kukusanyia Mapato zilizoko katika baadhi ya Vituo vya kukusanyia mapato ambapo ametembelea maeneo ya Geti la Kapalala, Geti la Mtapenda, na Soko la Mnyaki katika Kata ya Katumba ili kubaini iwapo Mashine hizo zinatumika ipasavyo.

Katika ukaguzi huo Bw.Swai amesisitiza juu ya umuhimu

wa kujengewa uelewa Watoza Ushuru wanaotumia Mashine hizo ili waweze kuzitumia kama inavyotakiwa ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa Mashine hizo zinakuwa Online muda wote zikiwa zinakusanya mapato ili Taarifa za Mapato ziweze kusoma kwa wakati kwenye Mfumo wa kukusanyia Mapato TAMISEMI.



***Pichani: Afisa TEHAMA Mkoa wa Katavi Bw.Curthbert Swai (Mwenye Shati la Kitenge) akipokea maelezo kutoka kwa Mmoja wa watoza ushuru katika soko la Mnyaki Katumba (Mwenye Kikoti kushoto) lipotembelea baadhi ya vituo vya Ukusanyaji wa Mapato kwa lengo la kujionea namna ambayo Watoza Ushuru katika baadhi ya maeneo Nsimbo wanatumia Mashine za Ukusanyaji wa Mapato Februari 15, 2019. (Picha na John Mganga)***

Jarida hili la Wiki Nsimbo huandaliwa na kutolewa na  
Kitengo cha Teknolojia ya Habari Mawasiliano na  
Uhusiano Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji ,Halmashauri  
ya Wilaya ya Nsimbo,Ofisi Na.2

**Mawasiliano:**

Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo

SLP 688,Mpanda Katavi

Barua pepe:[info@nsimbodc.go.tz](mailto:info@nsimbodc.go.tz)

Tovuti:[www.nsimbodc.go.tz](http://www.nsimbodc.go.tz)

Tel +25546310716